# YUSUFU

# NINA NDOTO

## NDOTO YAKO, MAISHA YAKO

**Anzia Hapo Ulipo, Anza na Ulichonacho.**

Edius Katamugora

**YUSUFU NINA NDOTO**

**©Haki ya kunakili: Edius Katamugora**

Hakuna sehemu yoyote ya kitabu hiki ambayo inaruhusiwa kutolewa upya au kuhamishwa kwa namna au njia yoyote; kielectroniki au kiufundi au kwa kutoa nakala (photocopy), kurekodi kwa namna ya kuhifadhi habari au kurudishia tena bila idhini ya mwandishi kwa

maandishi isipokuwa matumizi ya dondoo fupi fupi kwa lengo la kufundisha au kujifunza.

**ISBN**

**Chapa ya Kwanza 2019**

**Mawasiliano: Edius Katamugora**
**Barua Pepe: ekatamugora@gmail.com**

**Tovuti: www.bideism.blogspot.com**

**Simu: +255 764 145 476/ +255 758 594 893**

**Cover Design: Julius Sangawe (JGRAPHICS BRAND)**

**Type setting and layout design**

Kimechapwa na
**UTMOST INVESTMENT (T) COMPANY LIMITED**
Kongo/Ndovu Street
P.O.Box 6221, Dar es Salaam
Email: utmost.investment96@yahoo.com
Cell: +255 753 094 423, +255 653 131 627

## SIFA KUHUSU KITABU

**Umependelewa kuwa na ndoto,sio wote wataipenda na kuisapoti**

Yakobo alibahatika kuwa na watoto 12,wote walikuwa wa kiume, huenda walikuwa watulivu na watiifu kwa baba yao bado Yakobo alimpenda zaidi Yusufu.

Kupendwa sana kwa Yusufu hakukumfanya achukiwe na ndugu zake lakini ndoto aliyoiota na kuitamani iwe iliwakera wote na kumfanya aanze kuchukiwa hatimaye. Kitendo cha kuota Jua, mwezi na nyota 11 zikimuinamia kulitabiri kuwa baadaye atanyenyekewa na ndugu na hata wazazi wake, kulimaanisha pia ukuu atakaokuwa nao na pia yeye kuwa chanzo cha msaada kwa wengine.(Mwanzo 37:9)

Yawezekana wewe pia una ndoto,naam, yawezekana una maono ya kufanya makubwa hapo baadaye. Tambua kuwa hilo ni pendeleo, si wote wenye kutambua ndoto zao wanaochukua hatua kuzitimiza. Sio wote wanaojua kuwa "*Kumsaidia mwingine kutimiza ndoto yake ni kambo zuri lenye kuwasaidia wao pia kutimiza ndoto zao*".

Si vibaya, ni jambo jema zaidi lakini tambua kuwa ukubwa wa ndoto huenda sambamba na ukubwa wa changamoto/upinzani kutoka kwa wengine. Watu hodari hupambana kushinda vikwazo vinapoinuka lakini watu werevu na imara hujiweka tayari zaidi hata kukabili vipingamizi toka kwa watu wa karibu kama wazazi, wenza, ndugu na marafiki, *watu hawa wa karibu wana uwezo mkubwa sana kuua ndoto yako.*

Ni lazma uipambanie ndoto yako kwani ndoto ina tabia ya kuwavutia wengine hasa wenye mtazamo hasi kuielekea. Kuvutiwa kwao ni kule kutaka kushuhudia ikitoweka au kushindwa kutimia kupitia wewe, hivyo basi pendeleo la kuwa na ndoto linakulazimu kuwa imara huenda hata mara mbili zaidi kabla hujaitambua ndoto yako.

Kuna muda utapata sapoti kwa watu hata usiotarajia na tarajia kukosa sapoti kwa watu usiowadhania kama wataweza kushindwa kukusapoti. Mfano, nakumbuka tarehe 25 mwezi Agosti mwaka 2018, nilifanya uzinduzi wa kitabu changu cha kwanza kiitwacho Mawazo ya msafiri pale *Maktaba kuu ya Taifa.* Nilitaraji sapoti kubwa sana kwa jinsi ambavyo nilisapoti shughuli nyingine za uzinduzi wa vitabu, *network* kubwa niliyonayo na hata marafiki niliowaweka karibu zaidi lakini mambo yakawa tofauti kabisa. Nilipokea simu nyingi zisizo na sababu

ya msingi ya kutokufika kwao kwenye shughuli yangu, simu nyingi zilinivunja moyo, naam, waalikwa wengi hawakuitikia mwaliko wangu. Jambo la kushangaza ni kuwa wale ambao sikuwaalika, waliweza kufika eneo la tukio wakidai kuwa wamepata taarifa mitandaoni. Kuna mwalimu wangu alikuwepo upande wa pili wa maktaba lakini nilipotoka nje nikakumbana nae mlangoni, baada ya kumueleza kinachojiri, alifurahi sana, aliwaita wenzake wawili na kujumuika nami, nakumbuka pia alinipatia kiasi cha fedha kusapoti kitabu changu. Ni hapa nilipoukumbuka usemi wa gwiji Albert Einstein aliposema, *"Ukitaka kuwa na furaha, unganisha furaha na lengo au ndoto wala sio watu au vitu"*. Ndoto yangu ilikuwa ni kuzindua kitabu wala sio kupewa sapoti na waalikwa siku ya uzinduzi.

Lengo kuu la ujio wa Yesu kristo hapa duniani lilikuwa ni kuuokoa ulimwengu dhidi ya shetani, naam, ilikuwa kuwakomboa wanadamu kutoka kwenye dhambi ya urithi na hali ya kutokukamilika mpaka kwenda kwenye uhai udumuo milele, lakini sio wote waliompokea, sio wote waliomuunga mkono au kuthamini upendo wake, wengi wao walimpinga na hatimaye kumuua kabisa.

Unapokosa sapoti au msaada wa kutimiza ndoto yako, usihuzunike wala usikate tamaa.

Niliwahi kuandika kwenye kitabu changu kiitwacho **Mawazo ya msafiri** kuwa kuna faida unapokumbana na changamoto na vikwazo hasa pale unapokosa msaada kabisa, faida hizo hutia ndani:

- *Kudhihirisha uhalisia uliopo ndani yetu.* Kama ambavyo kisu au kiwembe kinatukata mwilini na damu kutoka, ndivyo ambavyo tunajua uhalisia wa ndani yetu. Huenda una nguvu fulani ambayo hata wewe mwenyewe huijui, lakini kikwazo kinachokukabili kitadhihirisha uwezo ulionao ndani yako. Mfano, kupitia kukabwa na wahuni au kukutana na mnyama mkali anayedhuru, kunaweza kukufanya ukakimbia umbali mrefu na kwa kasi kuliko ulivyotaraji kuwa unaweza.
- *Kuimarika zaidi.* Muda ambao baba amekimbiwa na mkewe huwezesha kujifunza mbinu mbalimbali za kuihudumia familia kama vile kupika, kufua nguo na kupasi, kuandaa watoto wa shule, kufanya usafi na vitu vinginevyo ambavyo asingevijua kama asingekimbiwa na mama. Vilevile, mama mjane au aliyekimbiwa na mume hujifunza pia kuishi kwa kujitegemea na kwa umakini zaidi hali ambayo asingejifunza kama tu asingekutana na changamoto hiyo.
- *Kuongezeka kwa ubunifu. Huu ni ukweli usiopingika kuwa, maendeleo yaliyopo leo, hasa katika sayansi na teknolojia*

yalisababishwa na kuwepo kwa vikwazo fulani awali. Uhitaji wa kutatua vikwazo hivi ndio umepelekea watu kugundua njia mbadala za kutatua vikwazo hivyo na kuongezea ubunifu pale palipohitajika.

- Kutujuza maana ya maisha. Maisha bila vikwazo ni sawa na barabara ndefu isiyo na kona, kamwe haiwezi kumvutia dereva wa chombo cha usafiri au kumfanya aongeze umakini. Changamoto na vikwazo mbalimbali ndivyo vinavyofanya kila siku tuamke mapema na kuchelewa kulala usiku kwa lengo tu la kuitimiza ndoto tuliyonayo.
- Kutuleta karibu zaidi na Mungu. Kwa wasomaji wa vitabu vya dini watakubaliana na msafiri anaposema kuwa, vikwazo humfanya mtu awe karibu zaidi na Mungu. Manabii mbalimbali na mitume walimkaribia zaidi Mungu wao kipindi walichokabiliana na vikwazo. Waisraeli walipokuwa utumwani Misri walimlilia sana Mungu wao, leo hii matatizo mengi kama magonjwa, ugumu wa maisha kiuchumi na uhitaji wa faraja umepelekea watu wengi kujaa makanisani na misikitini, wanaamini kuna faraja sehemu hizo, wanaamini kuwa huu ni muda sahihi wa kumrudia Mungu kutokana na vikwazo vinavyowakabili na kushikwa na kiu ya kutimiza ndoto walizonazo.

Kama kweli unaipenda na umedhamiria kuitimiza ndoto yako, vikwazo haviwezi kamwe kukuzuia kutimiza malengo yako, kukosa msaada au sapoti toka kwa watu fulani uliowatarajia, si sababu ya wewe kushindwa kuitimiza ndoto yako. Njia pekee ya kutokujuta hapo baadaye ni kuifuata ndoto yako na kuitimiza. Ni maumivu yaliyoje kushindwa kuifuatilia ndoto yako eti kwa sababu tu wengine hawaiungi mkono.

– Erick Gamba, mwandishi kitabu cha *Mawazo ya Msafiri*

Ningekua na nguvu ya kulazimisha, ningewalazimisha watu wote walambe asali inayopatikana ndani ya kitabu hiki.

–William Bhoke, mwandishi kitabu cha *Usikate Tamaa Katika Maisha: Ulizaliwa Kushinda na Sio Kushindwa.*

Kitabu hiki ni hazina kubwa kwa kila mwenye ndoto. Kama kuna rafiki mmoja ambaye unapaswa kuwa naye basi ni kitabu hiki. Ukilala, lala nacho. Ukiamka, amka nacho. Ukitembea tembea nacho. Ukifuata kilicho humu na kukitekeleza maishani mwako, watakuona ukivuka ng'ambo.

–Godius Rweyongeza mwandishi wa *Tatizo Si Rasilimali Zilizopotea.*

Kitabu hiki ni mwongozo ulosubiriwa kwa kila mtu mwenye kiu kubwa ya kuishi maisha yenye maana na ya kuacha alama kwa wengine. Mwanzo wa maisha bora na kuwa alama njema kwa wengine

huanza na ndoto. Ndoto ndio hatua ya kwanza ya kuanza hapo hapo ulipo kuona mwendo mrefu wa kule unakojiona baada ya muda fulani.

Habari za Yusufu kuwaambia ndugu zake habari ya ndoto aloiota ni mwaliko wa kila mmoja kutodharau ndoto yake vile atakavyoona baadaye. Ndoto ni dira na msukumo ambao kila mmoja mwenye ndoto huwa haachi kuipambania na kuwa na tumaini kuwa ipo siku itakuwa dhahiri.

Kila mmoja ana nafasi ya kuota ndoto na kuweza kuanza alipo kwa kuangalia nini alichonacho kinachoweza kumkaribisha karibu na picha ya ndoto yake.

Neno "nina ndoto" na "anzia ulipo na anza na ulichonacho" ni maneno ambayo yamenipa nguvu mimi mwenyewe kuwa kila kitu kinachohitajika kusogea hatua kubwa ya maisha ipo ndani yangu. Hili linahimiza umuhimu wa kuwa na ndoto, kuanza na nilivyonavyo na kuanzia nilipo sasa.

Kitabu hiki kitaendelea kuwa na faida zaidi kadri utakavyokuwa unasoma, kurudia kusoma na kuchambua kwa kina vipi maisha yako ujiangalie ulipo na ndoto yako ni ipi.

– Dkt. Raymond N Mgeni.

## SHUKRANI

"Hakuna jukumu linalohitajika kufanyika haraka kama kurudisha shukrani," alisema James Allen. Kwa msingi huo namshukuru Mungu aliyeniwezesha na kujaza hazina ya maandishi ndani yangu na pia kuniwezesha kutimiza ndoto ya kukamilisha kitabu hiki.

Kidole kimoja hakivunji chawa, kuna watu ambao bila nguvu zao kuwepo kazi hii ingelikuwa ngumu sana kwangu, watu hao wamefanya kazi hiyo kuwa rahisi sana kwangu. Nawashukuru sana wazazi wangu Bw. Jacob Kaijage na Bi. Revina Kawamala ambao wamekuwa daima mstari wa mbele katika kunisaidia kuendeleza kipaji hiki cha uandishi.

Pili, namshukuru sana Padre Dkt. Faustin Kamugisha kwa kuandika maneno yaliyo nyuma ya kitabu hiki. Namshukuru sana kwani mara zote huwa ananitia moyo na kuniambia, "Usiache kuandika." Maneno hayo kila siku unifanya kuwa bora zaidi.

Nawashukuru pia, Jamhuri Media Ltd, wanaochapisha gazeti la JAMHURI ambao walianza kurusha makala za 'NINA NDOTO' katika gazeti ambazo leo hii zimezaa kitabu hiki.

Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru rafiki zangu William Bhoke, Shukrani Bwire, Dativa Matungwa na Antia Mutapima, nilipowaambia naandika kitabu hiki, kila siku hamkuchoka kunitia moyo na hatimaye nimeweza kukamilisha kitabu hiki. Nakubaliana na Pat Morley aliyesema, "Kutiwa moyo ni chakula cha moyo, na kila moyo ni moyo wenye njaa." Nawashukuru wote walionitia moyo kuandika kitabu hiki.

Aidha namshukuru pia Julius Sangawe kwa kubuni jarada zuri sana lililotumika katika kitabu hiki.

Naunga mkono hoja ya Timothy Foote aliyesema "Kila mtu anahitaji mhariri." Kwa msingi huo namshukuru ndugu Zeri Mwakabona kwa kuhariri vyema kitabu hiki.

Nawashukuru waandishi hawa; William Bhoke, Dkt. Raymond Mgeni, Erick Gamba na Godius Rweyongeza, ambao walikubali kupitia kitabu hiki na kuandika neno kuhusu kitabu hiki, nasema asante sana.

Mwisho nikushukuru wewe mpendwa msomaji kwa kununua kitabu hiki. Nitakuwa na furaha na faraja nikisikia kwamba baada ya kusoma kitabu hiki umeweza kusema, "Nitafanya kitu fulani kuhakikisha ndoto zangu zinatimia." Yote yakishasemwa ndugu msomaji usikose kusoma vitabu vyangu vingine kama BARABARA YA MAFANIKIO na NAMNA YA KUWA MTAALAMU UKIWA BADO UNASOMA.

## UTANGULIZI

**"Kama kuna kitabu ambacho unahitaji kukisoma, lakini bado hakijaandikwa unatakiwa kukiandika,"** alisema Toni Morrison. Usemi

huu ndio umekuwa mwongozo, nguzo na msukumo wa kuandika kitabu hiki.

Nimesoma na kusikia mambo mengi yanayohusu ndoto na namna ya kuzitimiza lakini kuna mambo mengi nilitamani kuyasoma na kuyasikia lakini bado masikio yangu hayakupata kusikia wala macho yangu hayakupata kuona, kwa msingi huo kitabu hiki cha YUSUFU NINA NDOTO kikazaliwa.

Kitabu hiki kimeandikwa kwa mfumo wa makala ambazo ndani yake mawazo tofauti tofauti yalizaliwa ili kuipa maana ndoto.

Muhusika mkuu wa kitabu hiki ni Yusufu wa agano la Kale ambaye alikuwa na ndoto toka akiwa na umri wa miaka 17.

Ndoto ya Yusufu inakumbwa na vikwazo, vingingi na matatizo lukuki, lakini mwisho wa siku ndoto yake inakuja kutimia.

Kisa cha Yusufu kinaonesha kwamba si wewe pekee unayepitia katika matatizo, matatizo anayapitia karibia kila mtu isipokuwa kuna wanaobadili matatizo kuwafanya washindi na kuna wale ambao wanakumbatia matatizo na kuishi nayo milele. **"Taabu huwafanya baadhi ya watu kuvunjika moyo na wengine kuvunja rekodi,"** alisema William Arthur Ward mtunzi wa vitabu.

**"Matatizo si tatizo, matatizo ni daraja,"** kama anavyosema rafiki yangu Padre Dk. Faustin Kamugisha, mwandishi maarufu wa vitabu vya kutia hamasa. Matatizo, mikikimikiki na vikwazo ni njia ya kukupeleka kwenye hatima yako. **"Kama hautatui tatizo, wewe ni tatizo,"** anakazia mchungaji na mwandishi Sunday Adelaja.

Kisa cha Yusufu kina mengi ya kutufunza, ukitaka kutimiza ndoto zako, kaa kimya na usipige kelele watu wataona matokeo, kuwa na maono yaliyobebwa na malengo, ambatana na watu wenye ndoto maana ndege wenye mabawa yanayofanana huruka pamoja, jali muda, **"Ukiua muda unaua fursa,"** kama usemavyo msemo wa Kiafrika.

Kuwa na ndoto kubwa na ishi maisha ya ndoto yako. Daima kumbuka umezaliwa kwa sababu, Mungu haumbi mtumba. Linda ndoto yako isipotee kama kufuli linavyolinda mlango. Usikubali ndoto yako ife wakati bado unaishi. Nakubaliana na hoja ya Norman Cousines aliyesema, **"Kifo sio hasara kubwa maishani. Hasara kubwa ni ile inayokufa ndani yetu wakati tunaishi."**

Kuna muda unaweza kutupwa kwenye shimo kama Yusufu, kumbe shimo ulilowekwa lipo karibia na njia ya kwenda Misri ambako hatima yako itatimilizika. Kuna muda unaweza kufikiri, umezikwa kumbe umepandwa.

Jenga tabia ya kujiongezea thamani. Kila siku jiulize, "Nitawezaje kujiongezea thamani leo?" Jiulize mambo unayotakiwa kuyafanya kila siku ili uhakikishe unasonga mbele zaidi na si kurudi nyuma. Ukijipa thamani ndogo, uwe na uhakika dunia haitapandisha thamani yako. Jipe thamani lakini usijikweze.

Ninakubaliana na Martin Luther King Jr. aliyewahi kusema, **"Ukishindwa kupaa, kimbia. Ukishindwa kukimbia, tembea. Ukishindwa kutembea, tambaa. Katika kila unachokifanya hakikisha**

**unapiga hatua fulani.''** Kuna wakati unafika na hakuna mtu yeyote anayekuhamasisha, kukutia moyo ama kukuunga mkono, mtu unayemwitaji ni wewe pekee.

Waache watu wakushushie thamani. Usikubali hata siku moja wewe kujishushia thamani.

Ndugu zake Yusufu waliona kijana mwenye ndoto za Alinacha wakampa jina la ''Bwana Ndoto.''
Waliomnunua (Waishmaeli) waliona mtumwa wa kwenda kuuzwa.
Potifa aliona anafaa kuwa kijakazi wake wa ndani.
Mke wa Potifa, akida wa Farao, mkuu wa askari, aliona anafaa kuwa mchepuko.
Askari wa gereza waliona mfungwa kama walivyo wafungwa wengine.
Farao aliona kiongozi anayepaswa kuwa Waziri Mkuu katika nchi yake. Nchi ya Misri.

Yusufu aliuzwa na ndugu zake kwa Waishmaeli kwa vipande ishirini vya fedha. Vipande ishirini vya fedha kilikuwa ni kiwangi cha kuuza mtumwa wa kike si wa kiume (Hii ilikuwa sheria iliyoweka na mfalme wa Babylon alliyeitwa Hammurabi). Uzito wa kipande kimmoja ni gramu 8.33 hivyo vipande ishirini ni gramu 166.6, ambapo gramu moja ni sawa na dola za Kimarekani 0.54 ambayo ni sawa na laki mbili na elfu sitini na tisa. Ndugu zake walimdharau vya kutosha lakini yeye hakuwahi kujidharau. Walimshusha thamani na kumuuza kama mtumwa wa kike lakini yeye hakuwahi kujishusha thamani. Jithamini, jikubali, kuwa wewe.

Waache watu wakuchukulie poa na kawaida. Usikubali hata siku moja kujichukulia poa. Wewe ni mwenye thamani. Wewe ni dhahabu. Wewe

ni lulu. Wewe ni mti wenye matunda. Watu wakikurushia mawe yaokote ujenge msingi imara ili siku wakirudi wakute umesimama mahali imara.

Soma kitabu hiki kwa umakini mkubwa na yale utakayoyapata yaweke katika matendo, wanasema, muungwana ni vitendo. Matokeo makubwa hayatatokea usipoweka katika matendo yale uliyojifunza. Daima jifunze kwa kufanya ndipo utakapofika mbali.

Nakutakia usomaji mwema,

Rafiki yako,
Edius Katamugora (Kijana wa Maarifa)
10/12/2019

**KISA**

Kitabu hiki kimeandikwa kutokana na kisa cha Biblia kinachozungumzia juu ya maisha ya Yusufu mwana wa Yakobo.

Yusufu alikuwa mwenye miaka kumi na saba, alipokuwa akichunga kondoo pamoja na ndugu zake; naye alikuwa kijana mdogo pamoja na wana wa Bilha, na wana wa Zilpa, wake wa baba yake. Yusufu alikuwa akimletea baba yao habari zao mbaya. Basi Israeli akampenda Yusufu kuliko wanawe wote, maana ni mwana wa uzee wake, akamfanyia kanzu ndefu. Ndugu zake wakaona ya kuwa baba yao anampenda kuliko ndugu zake wote, wakamchukia, wala hawakuweza kusema naye kwa amani.

Yusufu akaota ndoto, akawapa ndugu zake habari, nao wakazidi kumchukia. Akawaambia, "Tafadhalini, sikieni ndoto hii niliyoiota. Tazama, sisi tulikuwa tukifunga miganda shambani, kumbe! Mganda wangu ukaondoka, ukasimama, na tazama, miganda yenu ikazunguka ikainama mbele ya mganda wangu." Ndugu zake wakamwambia, "Je, kweli wewe utatumiliki sisi? Nawe utatutawala sisi?" wakazidi kumchukia kwa ajili ya ndoto yake, na maneno yake.

Akaota tena ndoto nyingine, akawaambia ndugu zake, akasema, "Angalieni, nimeota ndoto nyingine; na tazama, jua na mwezi na nyota kumi na moja zikaniinamia." Akamwambia baba yake

na ndugu zake; baba yake akamkemea akamwambia, "Ni ndoto gani hii uliyoiota? Je, mimi na mama yako na ndugu zako tutakuja tukusujudie hata nchi?" Ndugu zake wakamhusudu; bali baba yake akalihifadhi neno hili moyoni mwake.

Ndugu zake wakaenda kuchunga kondoo za baba yao huko Shekemu. Israeli akamwambia Yusufu, "Je, ndugu zako hawachungi kondoo katika Shekemu? Njoo, nikutume kwao." Akamwambia, "Mimi hapa."

Akamwambia, "Enenda, basi, ukaone kama ndugu zako hawajambo, na kundi nalo li salama, ukaniletee habari." Basi akampeleka kutoka bonde la Hebroni, akafika Shekemu.

Mtu mmoja akamkuta, naye alikuwa anazungukazunguka katika nyika, yule mtu akamwuliza, akisema, "Unatafuta nini?" Akasema, "Nawatafuta ndugu zangu; tafadhali uniambie mahali wanakochunga." Yule akasema, "Wametoka hapa, maana niliwasikia wakisema, 'Twendeni Dothani,'" Basi Yusufu akawafuata ndugu zake akawakuta huko Dothani. Wakamwona toka mbali, na kabla hajawakaribia, wakafanya shauri juu yake ili wamwue. Wakasemezana wao kwa wao, "Tazama, yule bwana wa ndoto anakuja! Haya twende, tukamwue na kumtupa katika birika mojawapo, nasi tutasema, "Mnyama mkali amemla'; kisha tutaona zitakuwaje ndoto zake!" Reubeni akasikia akamwokoa katika mikono yao, akasema, "Tusimwue." Reubeni akawaambia, "Msimwage damu; mtupeni katika birika hii iliyopo nyikani, wala msimguse"; ili apate kumwokoa katika mikono yao, akamrudishe kwa baba yake.

Ikawa Yusufu alipofika kwa ndugu zake, wakamvua Yusufu kanzu yake, kanzu ile ndefu aliyoivaa, wakamtwaa wakamtupa katika birika; na hiyo birika ilikuwa tupu, hamna maji. Nao wakakaa kitako kula chakula; wakainua macho yao, wakaona msafara wa Waishmaeli

wanakuja wakitoka Gileadi na ngamia zao, wakichukua ubani na zeri na manemane, wakisafiri kuvichukua mpaka Misri. Yuda akawaambia ndugu zake, "Kwafaa nini kumwua ndugu yetu, na kuificha damu yake? Haya, na tumwuze kwa hawa Waishmaeli, wala mikono yetu isimdhuru, maana yeye ni ndugu yetu na damu yetu." Ndugu zake wakakubali.

Wakapita wafanyabiashara Wamidiani; basi wakamtoa Yusufu, wakampandisha kumtoa katika birika, wakamwuza kwa Waishmaeli kwa vipande vya fedha ishirini; nao wakamchukua Yusufu mpaka Misri. Akarudi Reubeni birikani, kumbe! Yusufu hayumo katika birika akararua nguo zake. Akarudi kwa ndugu zake, akasema, "Mtoto hayupo, nami niende wapi?" Wakaitwaa kanzu ya Yusufu, wakamchinja mwanambuzi, na kuichovya kanzu katika damu. Wakaenda nayo ile kanzu ndefu, wakamletea baba yao, wakasema, "Tumeona hii; basi utambue kanzu hii ni ya mwanao, ama siyo." Akaitambua, akasema, "Ndiyo kanzu ya mwanangu, mnyama mkali amemla; bila shaka Yusufu ameraruliwa." Yakobo akararua mavazi yake, akajivika gunia viunoni na kumlilia mwanawe siku nyingi. Wanawe wote, na binti zake wote, wakaondoka wamtulize, lakini akakataa kutulizwa, akasema, "La! nitamshukia mwanangu, nikisikitika, hata kuzimu." Baba yake akamlilia.

Nao Wamidiani wakamwuza huko Misri, kwa Potifa, akida wa Farao, mkuu wa askari.

Basi Yusufu akaletwa mpaka Misri; naye Potifa, akida wa Farao, mkuu wa askari, mtu wa Misri, akamnunua mkononi mwa hao Waishmaeli waliomleta huko. Bwana akawa pamoja na Yusufu, naye akastawi; naye alikuwa katika nyumba ya bwana wake, yule Mmisri. Bwana wake akaona ya kwamba Bwana yu pamoja naye, na ya kuwa Bwana anafanikisha mambo yote mkononi mwake. Yusufu akaona neema machoni pake, akamtumikia. Naye akamweka awe msimamizi juu ya nyumba yake, na yote yaliyomo akayaweka mkononi mwake.

Ikawa tokea wakati alipomweka awe msimamizi juu ya nyumba yake, na vyote vilivyomo, Bwana akabariki nyumba ya yule Mmisri kwa ajili ya Yusufu. Mbaraka wa Bwana ukawa juu ya vyote alivyokuwa navyo katika nyumba, na katika shamba. Akayaacha yote aliyokuwa nayo mkononi mwa Yusufu; wala hakujua habari za kitu chochote chake, ila hicho chakula alichokula tu.

Naye Yusufu alikuwa mtu mzuri, na mwenye uso mzuri. Ikawa baada ya mambo hayo. Mke wa bwana wake akamtamani Yusufu, akamwambia, "Lala nami." Lakini akakataa, akamwambia mke wa bwana wake, "Tazama, bwana wangu hajui kitu kilichowekwa kwangu nyumbani, na vyote alivyo navyo amevitia mkononi mwangu. Hakuna mkuu katika nyumba hii kuliko mimi, wala hakunizuilia kitu chochote ila wewe, kwa kuwa wewe u mkewe. Nifanyeje ubaya huu mkubwa nikamkose Mungu?" Akawa akizidi kusema na Yusufu siku baada ya siku, lakini hakumsikia alale naye, wala aongee naye.

Ikawa, siku moja, akaingia nyumbani atende kazi yake, wala hapakuwa na mtu katika watu wa nyumbani humo ndani; huyo mwanamke akamshika nguo zake, akisema, "Lala nami." Yusufu akaiacha nguo yake mkononi mwake, akakimbia, akatoka nje. Ikawa alipoona ya kwamba amemwachilia nguo yake mkononi mwake, naye amekimbia nje, akawaita watu wa nyumbani mwake, akasema nao, akinena, "Angalieni, ametuletea mtu Mwebrania atufanyie dhihaka.

Ameingia kwangu, ili alale nami, nikalia kwa sauti kuu. Ikawa, aliposikia ya kuwa nimepaza sauti yangu na kulia, aliicha nguo yake kwangu, akakimbia, akatoka nje."

Basi akaiweka ile nguo hata bwana wake aje nyumbani. Naye akamwambia kama maneno hayo, akisema, "Yule mtumwa Mwebrania uliyeniletea kwetu, aliingia kwangu kunidhihaki. Ikawa nilipopaza sauti yangu, nikalia, akaacha nguo yake kwangu akakimbia nje." Ikawa bwana wake aliposikia maneno ya mkewe aliyomwambia, akisema, "Mtumwa wako amenitendea mambo kama haya!", hasira yake ikawaka.

Bwana wake akamtwaa Yusufu, akamtia gerezani, mahali walipofungwa wafungwa wa mfalme, naye akawamo humo gerezani. Lakini Bwana akawa pamoja na Yusufu, akamfadhili, akampa kibali machoni pa mkuu wa gereza. Mkuu wa gereza akawatia mkononi mwa Yusufu watu wote waliofungwa, waliomo gerezani; na yote yaliyofanyika humo ndiye aliyeyafanya. Wala mkuu wa gereza hakuangalia neno lililoko mkononi mwa Yusufu; kwa kuwa Bwana alikuwa pamoja naye. Bwana akafanikisha yote aliyoyafanya.

Ikawa, baada ya mambo hayo, mnyweshaji wa mfalme wa Misri, na mwokaji wake, wakamkosa bwana wao, mfalme wa Misri. Farao akawaghadhibikia maakida wake wawili, mkuu wa wanyweshaji na mkuu wa waokaji. Akawatia katika lindo nyumbani mwa mkuu wa askari,

humo gerezani, mahali alipofungwa Yusufu. Mkuu wa askari akamwekea Yusufu watu hao, naye akawahudumu, nao wakakaa siku kadha wa kadha katika kifungo.

Wakaota ndoto wote wawili, kila mtu ndoto yake usiku mmoja, kila mtu kwa tafsiri ya ndoto yake. Mnyweshaji na mwokaji wa mfalme wa Misri walifungwa gerezani. Yusufu akawajia asubuhi, akawaona wamefadhaika. Akawauliza hao maakida wa Farao, waliokuwa pamoja naye kifungoni, nyumbani mwa bwana wake, akisema, "Mbona nyuso zenu zimekunjamana leo?" wakamwambia, "Tumeota ndoto wala hapana awezaye kuifasiri." Yusufu akawaambia, "Kufasiri si kazi ya Mungu? Tafadhalini mniambie."

Mnyweshaji mkuu akamhadithia Yusufu ndoto yake; akamwambia, "Katika ndoto yangu nimeota, uko mzabibu mbele yangu. Na katika mzabibu mlikuwa na matawi matatu, nao ulikuwa kama unamea, unachanua maua, vishada vyake vikatoa zabibu zilizoiva. Na kikombe cha Farao kilikuwa mkononi mwangu, nikazitwaa zabibu, nikazikamua katika kikombe cha Farao, nikampa Farao kikombe mkononi mwake."

Yusufu akamwambia, "Tafsiri yake ndiyo hii. Matawi matatu ni siku tatu. Baada ya siku tatu Farao atakiinua kichwa chako, atakurudisha katika kazi yako; nawe utampa Farao kikombe mkononi mwake. Kama desturi ya kwanza, ulipokuwa mnyweshaji wake. **Ila unikumbuke mimi, utakapopata mema, ukanifanyie Fadhili, nakuomba, ukanitaje kwa Farao, na kunitoa katika nyumba hii. Kwa sababu hakika niliibiwa kutoka nchi ya Waebrania, wala hapa sikutenda neno lolote hata wanitie gerezani."**

Mkuu wa waokaji alipoona ya kwamba hiyo tafsiri ni ya mema, akamwambia Yusufu, "Mimi kadhalika nilikuwa katika ndoto yangu, na tazama, ziko nyungo tatu za mikate myeupe juu ya kichwa changu. Na katika ungo wa juu, mlikuwa na kila namna ya chakula cha Farao,

kazi za mwokaji; ndege wakavila katika ungo juu ya kichwa changu.'' Yusufu akajibu, akasema, ''Tafsiri yake ndiyo hii. Nyungo tatu ni siku tatu. Baada ya siku tatu Farao atakiinua na kukuondolea kichwa chako, na kukutundika juu ya mti, na ndege watakula nyama yako.''

Ikawa siku ya tatu, siku ya kuzaliwa kwake Farao, akawafanyia karamu watumwa wake wote; akakiinua kichwa cha mkuu wa waokaji, miongoni mwa watumwa wake. Akamrudisha mkuu wa wanyweshaji katika kazi yake ya kunywesha, naye akampa Farao kikombe mkononi mwake. Bali akamtundika mkuu wa waokaji kama Yusufu alivyowafasiria. Lakini huyo mkuu wa wanyweshaji hakumkumbuka Yusufu, alimsahau.

Ikawa, mwisho wa miaka miwili mizima, Farao akaota ndoto; na tazama, amesimama kando ya mto. Na tazama, ng'ombe saba wazuri, wanono, walipanda kutoka mtoni, wakajilisha manyasini. Na tazama, ng'ombe saba wengine wakapanda nyuma yao kutoka mtoni, wabaya, wamekonda, wakasimama karibu na wale ng'ombe wengine ukingoni mwa mto. Kisha hao ng'ombe wabaya waliokonda wakawala wale ng'ombe saba wazuri, wanono. Basi Farao akaamka.

Akalala, akaota ndoto mara ya pili. Tazama, masuke saba yalimea katika bua moja, makubwa, mema. Na tazama, masuke saba membamba, yamekaushwa na upepo wa mashariki, yakatokeza

baada yao. Kisha hayo masuke membamba saba yakayala yale masuke saba makubwa yaliyojaa.

Basi Farao akaamka, kumbe! Ni ndoto tu.

Hata asubuhi roho yake ikafadhaika; akapeleka watu kuwaita waganga wote wa Misri, na watu wote wenye hekima walioko. Farao akawahadithia ndoto yake, wala hakuna aliyeweza kumfasiria Farao mambo hayo. Basi mkuu wa wanyweshaji akamwambia Farao akisema, Nayakumbuka makosa yangu leo. Farao aliwakasirikia watumwa wake, akanitia nifungwe nyumbani mwa mkuu wa askari, mimi na mkuu wa waokaji. Tukaota ndoto usiku mmoja, mimi na yeye; kila mtu kwa tafsiri ya ndoto yake tukaota. Na huko pamoja nasi palikuwa na kijana; Mwebrania, mtumishi wa mkuu wa askari, tukamhadithia, naye akatufasiria ndoto zetu; akamfasiria kila mtu kama ilivyokuwa ndoto yake. Ikawa, kama vile alivyotufasiria ndivyo ilivyotokea; mimi nalirudishwa katika kazi yangu, na yeye mwokaji alitundikwa.

**Ndipo Farao akapeleka watu, akamwita Yusufu, wakamleta upesi kutoka gerezani. Akanyoa, akabadili nguo zake, na kuingia kwa Farao.** Farao akamwambia Yusufu, Nimeota ndoto, wala hakuna awezaye kunifasiria; nami nimesikia habari zako, ya kwamba, usikiapo ndoto, waweza kuifasiri.Yusufu akamjibu Farao, akisema, "Si mimi; Mungu atampa Farao majibu ya amani." Farao akamwambia Yusufu, "Katika ndoto yangu nalikuwa nikisimama ukingoni mwa mto; na tazama, ng'ombe saba wanatoka mtoni, wanono, wazuri, wakajilisha manyasini. Kisha, tazama, ng'ombe saba wengine wakapanda baada yao, dhaifu, wabaya sana, wamekonda; katika nchi yote ya Misri sijaona kama hao kwa udhaifu. Na hao ng'ombe waliokonda, wabaya, wakawala wale ng'ombe saba wa kwanza, wale wanono. Na walipokwisha kuwala haikutambulikana ya kwamba wamewala, bali wakaonekana wabaya kama kwanza. Basi nikaamka. Kisha nikaona katika ndoto yangu, na tazama, masuke saba yanatokeza katika bua moja, mema, yamejaa. Na tazama, masuke saba membamba, dhaifu, yamekaushwa na upepo wa mashariki, yakatokeza baada yao. Na hayo masuke dhaifu yakameza

yale masuke saba mema. Nami nikawaambia hao waganga, wala hakuna aliyeweza kunionyesha maana yake.''

Yusufu akamwambia Farao, ''Ndoto ya Farao ni moja; Mungu amemwonyesha Farao atakayoyafanya hivi karibu. Wale ng'ombe saba wema ni miaka saba; na yale masuke saba mema ni miaka saba. Ndoto ni moja. Na wale ng'ombe saba, dhaifu, wabaya, waliopanda baada yao, ni miaka saba; na yale masuke saba matupu yaliyokaushwa na upepo wa mashariki, yatakuwa miaka saba ya njaa. Ndivyo nilivyomwambia Farao, ya kwamba Mungu amemwonyesha Farao atakayoyafanya hivi karibu. Tazama, miaka saba ya shibe inakuja, katika nchi yote ya Misri. Kisha kutakuja miaka saba ya njaa baada yake; na shibe ile yote itasahauliwa katika nchi ya Misri, na njaa itaiharibu nchi. Wala shibe ile haitajulikana katika nchi kwa sababu ya njaa inayokuja baadaye, maana itakuwa nzito sana. Na ndoto ya Farao kwa vile ilivyokuja mara mbili, ni kwa sababu neno hilo Mungu amelithibitisha, na Mungu atalitimiza upesi.

Basi, Farao na ajitafutie mtu mwenye akili na hekima amweke juu ya nchi ya Misri. Farao na afanye hivi, tena akaweke wasimamizi juu ya nchi, na kutwaa sehemu ya tano katika nchi ya Misri, katika miaka hii saba ya kushiba. Na wakusanye chakula chote cha miaka hii myema ijayo, wakaweke akiba ya nafaka mkononi mwa Farao wakakilinde kuwa chakula katika miji. Na hicho chakula kitakuwa akiba ya nchi kwa ajili ya miaka hiyo saba ya njaa, itakayokuwa katika nchi ya Misri, nchi isiharibike kwa njaa.''

Neno hilo likawa jema machoni pa Farao, na machoni pa watumwa wake wote. Farao akawaambia watumwa wake, Tupate wapi mtu kama huyu, mwenye roho ya Mungu ndani yake?

Farao akamwambia Yusufu, **"Kwa kuwa Mungu amekufahamisha hayo yote, hapana mwenye akili na hekima kama wewe. Basi wewe utakuwa juu ya nyumba yangu, na kwa neno lako watu wangu watatawaliwa. Katika kiti cha enzi tu nitakuwa mkuu kuliko wewe."**

*Farao akamwambia Yusufu, Tazama, nimekuweka juu ya nchi yote ya Misri. Farao akavua pete yake ya muhuri mkononi mwake, akaitia mkononi mwa Yusufu; akamvika mavazi ya kitani nzuri, na kumtia mkufu wa dhahabu shingoni mwake. Akampandisha katika gari lake la pili alilokuwa nalo. Na watu wakapiga kelele mbele yake, "Pigeni magoti."*

Hivyo akamweka juu ya nchi yote ya Misri. Farao akamwambia Yusufu, "Mimi ni Farao, na bila amri yako, mtu asiinue mkono wala mguu katika nchi yote ya Misri." Farao akamwita Yusufu, Safenath-panea; akamwoza Asenathi, binti Potifera, kuhani wa Oni, kuwa mkewe Yusufu akaenda huko na huko katika nchi yote ya Misri. Naye Yusufu alikuwa mwenye miaka thelathini, aliposimama mbele ya Farao, mfalme wa Misri.

Yusufu akatoka mbele ya uso wa Farao, akapita katika nchi yote ya Misri. Ikawa katika miaka ile saba ya shibe, nchi ikazaa kwa wingi. Akakusanya chakula chote cha miaka ile saba katika nchi ya Misri. Akaweka chakula katika miji; chakula cha mashamba yaliyouzunguka kila mji, akakiweka ndani yake. Yusufu akakusanya nafaka kama mchanga wa pwani, nyingi mno, hata akaacha kuhesabu, maana ilikuwa haina hesabu. Kabla ya kuja miaka ya njaa, Yusufu akazaliwa wana wawili, ambao Asenathi, binti Potifera, kuhani wa Oni, alimzalia. Yusufu akamwita jina lake yule aliyezaliwa kwanza, Manase, maana alisema, Mungu amenisahaulisha taabu zangu zote, na nyumba yote ya baba yangu. Na wa pili akamwita jina lake Efraimu, maana alisema, Mungu amenipa uzazi katika nchi ya mateso yangu.

Miaka ile saba ya shibe ikaisha katika nchi ya Misri, ikaanza kuja miaka ile saba ya njaa, kama vile Yusufu alivyosema. Kukawa na njaa katika nchi zote, bali katika nchi yote ya Misri palikuwa na chakula. Na nchi yote ya Misri ilipoona njaa, watu walimlilia Farao awape chakula. Farao akawaambia Wamisri wote, **"Enendeni kwa Yusufu; atakavyowaambia, fanyeni."** Njaa ikawa katika dunia yote pia. Yusufu akazifungua ghala zote, akawauzia Wamisri. Njaa ikawa nzito katika nchi ya Misri.

Watu wa nchi zote wakaja Misri kwa Yusufu; ili wanunue nafaka; kwa sababu njaa imekuwa nzito katika dunia yote.

**(Mwanzo 37, 39-41).**